## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/2 JULAI/AGOSTI 2018

**(a)Huku ukitoa mifano minne, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili. (al 4)**

- *Watoto wananyimwa haki licha ya katiba kulazimu haki hizi kutimizwa*
- *Mojawapo ya haki za kimsingi ni makazi ilhali watoto wanalala mitaani*
- *Watoto hawapati chakula ilhali wanatakiwa kupata lishe bora*
- *Wanaotakiwa kulinda haki za watoto ndio wanaozikiuka – kwa kuwapiga na kadhalika*
- *Wazazi na jamaa wa karibu wanashiriki katika unyanyasaji wa watoto*

**(b)Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. (al 3)**

- *Watoto hutekwa na kutumikishwa vitani*
- *Watoto hugeuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana*
- *Huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili*
- *Hulazimka kuvaa mabuti ya kijeshi/kubeba bunduki nzito(ambazo huwa nanga kwao kubeba)*

**(c)Kwa kurejelea aya ya nne , onyesha mchango wa serikali katika kuwajibikia haki za watoto. (al 3)**

- *Serikali ilikuwa na shabaha ya elimu kwa wote*
- *Kubuni sera ya elimu bila malipo*
- *Utekelezaji wa sera hii unaendelea*
- *Kunao wanaopigania haki ya kuwa na elimu bila malipo licha ya matatizo yaliyopo / Wanaong’ang’ania kuwepo kwa elimu bila malipo wanaonekana kana kwamba wanaota ndoto za mchana*

**(d)”wanaong’ang’ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana,” thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. (al 2)**

- *Asilimia ya watoto na watu wazima wasiojua kusoma bado ni kubwa*
- *Kuwepo kwa idadi kubwa ya watoto wasioenda shuleni*

- *Wazazi wanapojitahidi kujinyanyua na kujikuna wajipatapo kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wana wao, hujipata katika kinamasi hicho hicho cha ulitima.*
- *Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga*

(e)Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (al 3)

**(i)vigogo**

- *Walio katika mstari wa mbele,wapiganiaji haki watoto,mabingwa,wakereketwa,watawala*
- *Watetezi,wenye mamlaka, viongozi, wadau, wanaopenda kuendeleza elimu ya watoto*

**(ii)huwa nanga kwao**

*Huwa mazito kwao/ huwa mzigo kwao*

**(iii)kujikuna wajipatapo**

*Kujaribu kujinyanyua kwa uwezo wao, kujitahidi kulingana na uwezo wao*

**(a)Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno (40**)

i. Binadamu huishi kwa kutangamana
ii. Binadamu huathirika kitabia,kifikira,kimavazi na kimaisha
iii. Watu wote wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa
iv. Wanaoathiriwa Zaidi ni mahirimu wao na vijana
v. Hali ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika
vi. Watu wazima pia huathiriwa na wenzao
vii. Watu wote wanaweza kuathiriwa na shinikizo-rika
viii. Ni vigumu, kukabiliana na shinikizo-rika (alama 7, 1 ya utiririko)

**(b) Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho**

i. Shinikizo-rika hujitokeza kwa sura nyingi
ii. Hulazimisha watu kutenda kinyume na Imani yao
iii. Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kugengwa na wenzao

iv. Pia wanaweza kutishwa kwa kutumia mabavu

v. Wanaoshinikizwa wasimame kidete na watetee msimamo wao

vi. Wanasaikolojia wanapendekeza watu wajiamini

vii. Asiyejiamini atahangaishwa na wenzake (alama 6, 1 ya utiririko)

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Toa mifano miwili miwili ya (al.2)

**i.** Sauti ghuna ambazo ni vipasuo **/b/ /d/ /g/**

**ii.** Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo **/f/ /th/ /sh/ /h/**

(b) Onyehsa mofimu katika neno **Aliyemcha**

**a-nafsi/ngeli li-wakati ye-kirejeshi m-yambwa mtendewa ch-mzizi a-kiishio**

(c) Andika sentensi yenye muundo ufuatao (al.2)

KN(W+V) + KT (t +RH)

**Yule mtukutu alikuwa chini ya mti**

(d) Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja (al.2)

**Wafanyakazi wa shirika lile walifanya kazi kwa ushirikiano/kishirika**

(e) Kwa kutunga sentensi vumisha nomino ng'ombe kwa kivumishi cha idadi bainifu. (al.1)

**Ng'ombe sita wamepelekwa malishoni**

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendewa (al.1)

Mtoto wa waziri amekufa

**Waziri amefiwa na mtoto wake**

(g) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi (al.2)

Msomi hakutukuzwa siku hiyo

**Wasomi watakuwa wametuzwa siku hiyo**

(h) Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma (al.2)

**Kifaa cha madini**

**Tafuta pesa**

**Toa matunda mtini**

**Bakari alichuma matunda ya parachichi kwa kutumia kifaa kilichotengenezwa kwa chuma**

(i) Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo. (al.4)

Mwalimu mkuu hupigiwa nguo pasi na Maria

**Mwalimu mkuu – yambwa tendewa/kitondo**

**nguo –yambwa tendwa/kipozi**

**pasi – yambwa ala/ kitumizi**

**Maria - kiima**

(j) Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino (al.2)

**Nomino pekee (N)**

**Kiwakilishi (W)**

**N+U+N – Nomino +Kiunganishi +Nomino**

**N+V – Nomino + Kivumishi**

**N+V+V – Nomino + Kivumishi + Kivumishi**

**N+V+E – Nomino + Kivumishi + Kielezi**

**N+S – Nomino + Kishazi**

(k) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)

Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma

**Wageni hao na wengine walikula wali kwa nyuma**

(l) Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja (al.1)

**m-toto**

**m-tu**

(m) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo wingi (al.2)

Ng’ombe wangu ana ndama mdogo

**Vigombe vyangu vina vidama vidogo**

(n) Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo; (al.4)

i. Kishazi tegemezi na kishazi huru

**Mtoto aliyewasili leo** **amerudi kwao**

**K.T** **K.H**

ii. Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

**Angalilima kwa bidii** **angalivuna mavuno tele**

**K.T** **K.T**

(o) Eleza matumizi ya ‘ki’ katika sentensi ifuatayo: (al.3)

Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku


**kitoto – udogo**

**wakila , wakiimba – vitendo viwili kufanyika kwa wakati mmoja**

**kikasuku – ki ya kielezi**

(p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. (al.4)

Mtoto wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana




(q) Andika kwa msemo wa taarifa. (al.2)

‘Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili,’ Amina alipendekeza.

**Amina alipendekeza kuwa ilifaa wamwendee mama mkubwa ili awashauri juu ya jambo hilo**

(r) Andika kinyume cha: (al.1)

Chakula hiki kitamu nitakimeza

**Chakula hiki kichungu nitakitema**

(s) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo.

(i) Kiwakilishi nafsi huru

**Mimi hupika vizuri/sisi/wewe/nyinyi/yeye/wao**

(ii) Kiwakilishi nafsi kiambata

**A̲liondoka jana/wa/ni/tu/u/m**

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza sababu tano zilizochangia katika maenezi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki kabla ya Uhuru.

- ✓ Biashara kati ya pwani na bara
- ✓ Dini – kusambaza dini ya Uislamu na Ukristo
- ✓ Elimu – Wamishenari walitumia Kiswahili kufundisha kuandika, kusoma na kazi mbalimbali za ufundi
- ✓ Vyombo vya habari kama magazeti yalitumia Kiswahili
- ✓ Siasa – Wahusika wengi katika vita vya ukombozi walitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano
- ✓ Utafiti wa kina wa Madan, Steere na Krapf kuhusu Kiswahili na hata kuandika vitabu.

(b) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kuikuzalugha ya Kiswahili baada ya Uhuru nchini Kenya

- ✓ Kuundwa kwa kamati za elimu kama vile ya Ominde , Wamalwa, Gachathi, MaCkay, Kamunge na Koech
- ✓ Ongezeko la machapisho na vitabu vya Kiswahili
- ✓ Tamasha za michezo ya kuigiza na muziki kutumia Kiswahili
- ✓ Vyombo vya habari kutumia Kiswahili
- ✓ Kiswahili ni somo la lazima
- ✓ Kiswahili kutumika bungeni
- ✓ Kutumia Kiswahili katika sherehe za kitaifa
- ✓ Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya
- ✓ Vyuo vya kigeni kufunza Kiswahili
- ✓ Kiswahili ni somo la lazima suleni
- ✓ Kiswahili hutumika katika shughuli za kidini kama kuhubiri